

MAKAO MAKUU DODOMA

Habari zote Na Sifa Lubasi

HABARI LEO UKS.

Kichaa cha mbwa chaua watu 1,500 kila mwaka

UGONJWA wa kichaa cha mbwa husababisha vifo 1,500 kila mwaka nchini na watoto chini ya miaka mitano ndio wanaoathirika zaidi.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule alitoa kauli hiyo hivi karibuni wakati wa maadhimisho ya utoaji chanjo kwa mbwa ili kujikinga dhidi ya ugonjwa huo yaliyofanyika katika viwanja vya Mpunguzi jijini Dodoma.

"Kila mtu ambaye anafuga mbwa lazima afuate sheria na taratibu zake. Naagiza wataalamu wa mifugo wa wizara

na sekretarieti kutafuta suluhu ya mbwa wote wanaozurura mitaani. Mtu kama hawezi kufuata sheria, aache kufuga mbwa," alisema.

Alisema serikali inatekeleza mpango mkakati wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi katika kutoa chanjo hiyo kila mwaka ambapo mpaka sasa takribani mbwa 338,000 wameshachanjwa.

Senyamule alitaja lengo la dunia ni kutokomeza ugonjwa wa kichaa cha mbwa ifikapo mwaka 2030 kwa kuhakikisha kuwa kila mbwa anapatiwa chanjo kila mwaka.

"Naomba utaratibu huu uwe endelevu mpaka

ugonjwa huu uwe historia kwani Tanzania bila kichaa cha mbwa, inawezekana. Tunatakiwa kuzingatia chanjo pamoja na kupunguza idadi ya mbwa tunaofuga," alisema.

Naye Mkurugenzi wa Huduma za mifugo, Profesa Hezron Nonga, alisema Tanzania inakadiriwa kuwa na mbwa milioni 4.5 na paka milioni mbili wanaofugwa kwa malengo mbalimbali.

Alisema kwa mwaka kuna wastani wa matukio 2,030 ya mbwa wanaodhaniwa kuwa na kichaa. Hivyo Shirika la Afya Duniani (WHO), Shirika la Afya za Wanyama Duniani (WOAH) na Shirika la

Chakula na Kilimo (FAO) kwa pamoja wamekubaliana kutokomeza ugonjwa wa kichaa cha mbwa ifikapo mwaka 2030.

"Takwimu zinaonesha kuwa watu zaidi ya 60,000 hupoteza maisha kwa kichaa cha mbwa duniani kila mwaka. Kwa Tanzania, kila mwaka wastani wa matukio ya majeraha kwa binadamu yanayotokana na kuumwa na mbwa ni 3,387 na hii ni kwa mujibu wa ripoti ya WHO ya mwaka 2017," alisema.

Maadhimisho ya utoaji chanjo kwa mbwa na paka hufanyika kila mwaka duniani kote ikiwa ni kumuenzi muasisi wake, Dk

Luis Paster ambaye ndiye aligundua chanjo hiyo kwa wanadamu na mbwa kwa mara ya kwanza mwaka 1885.

Maadhimisho haya yanakwenda sambamba na utoaji wa chanjo ambapo kwa mwaka huu chanjo zaidi ya 60,000 zenye thamani ya Sh milioni 180 zimetolewa, lengo ni kuchanja mbwa kwa zaidi ya asilimia 70.

Maadhimisho ya mwaka huu yamebebwa na kaulimbiu inayosema; "Kichaa cha mbwa, afya moja, vifo sifuri" ikiwa na lengo la kutokomeza kabisa vifo vya binadamu vinavyotokana na ugonjwa wa kichaa cha mbwa.